

MAKOSA YA RUSHWA KATIKA CHAGUZI TANZANIA



AGOSTI 2009

MAKOSA YA RUSHWA KATIKA CHAGUZI TANZANIA

**Kimetayarishwa kwa ushirikiano kati ya POLICY FORUM
na TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA
(TAKUKURU)**

Kitabu hiki sio tafsiri ya neno kwa neno ya vifungu vyatia sheria mbalimbali zilizonukuliwa. Kwahiyoko tunaoomba kitabu hiki kisomwe pamoja na sheria husika kwa ajili ya rejea.

Mchoraji Katuni: Nathan Mpangala

ISBN 978-9987-9157-6-7

© Policy Forum 2009

Toleo la kwanza 2009

Toleo la pili 2010

DIBAJI

Policy Forum na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) tunakuletea tena chapisho hili la pili katika mtiririko wa machapisho yanayohusu elimu kwa umma juu ya kupambana na rushwa.

Mtakumbuka kuwa chapisho letu la kwanza la pamoja lilihusu sheria mpya namba 11 ya mwaka 2007 ya kuzuia na kupambana na rushwa hapa Tanzania,

Chapisho hili linaweka wazi sheria zetu zinavyosema kuhusu makosa ya rushwa katika chaguzi hapa nchini Tanzania na adhabu zinazotolewa kwa makosa husika,

Kwa kuzingatia kuwa tutakuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu 2009 na Uchaguzi Mkuu 2010 tunaamini chapisho hili litakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wakati wa chaguzi zetu hizi mbili muhimu.

Katika chapisho hili tumekusudia kuweka anwani na simu za ofisi zote za mikoa na Wilaya za TAKUKURU ili kuwarahisishia wananchi kuweza kuwasiliana na ofisi hizi pale tatizo lolote linapojitokeza.

Ni matumaini yetu kuwa mchakato ulioanzishwa na serikali wa kutunga sheria zingine kama sheria ya uhuru wa habari (Freedom of Information Act), ya vyombo vya habari (Media Services Act) na ile ya kuwalinda watoa taarifa (Whistle Blowers Protection Act) utaongeza nguvu na kasi katika mapambano dhidi ya rushwa nchini Tanzania.

**Semkae Kilonzo
Mratibu
Policy Forum**

YALIYOMO

1.0.	Utangulizi.....	1
2.0.	Isemavyo sheria ya uchaguzi wa kitaifa namba 1 ya 1985 kuhusu makosa ya rushwa katika uchaguzi.....	2
2.1.	Ushawishi wa rushwa kujiondoa kugombea	2
2.2.	Adhabu kwa hongo, kukirimu na kushinikiza.....	2
2.3.	Kosa la vitendo vya rushwa na uvunjaji wa sheria	4
2.4.	Vitendo vya rushwa na uvunjaji sheria	6
2.5.	Hongo, kukirimu au kushawishi kunakohusisha wajumbe au maafisa wa tume ya taifa ya uchaguzi	6
2.6.	Kuondolewa kwenye daftari kwa walioitiwa hatiani	7
2.7.	Makosa kwa maafisa wa uchaguzi.....	7
2.8.	Taarifa ya mahakama kuu kwa mkurugenzi wa uchaguzi kuhusu vitendo vya rushwa na uvunjaji sheria	7
3.0.	Isemavyo sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa namba 4 ya 1979 kuhusu rushwa katika uchaguzi.....	8
3.1.	Adhabu kwa watu wanaovunja sheria	8
3.2.	Watuhumiwa waliopatikana na hatia za rushwa na uvunjaji sheria kuondolewa kwenye daftari	8
4.0.	Isemavyo sheria namba 11 ya 2007 kuhusu makosa ya rushwa katika chaguzi.....	9
4.1.	Hongo na vitendo vya rushwa	9
4.2.	Rushwa ya ngono.....	10
4.3.	Kushiriki na kusaidia kutenda uovu	10
4.4.	Matumizi mabaya ya mamlaka.....	10
4.5.	Kula njama	10
4.6.	Kutumia ushawishi	11
5.0.	Anuani za ofisi za takukuru za mikoa na wilaya	12 /13

1.0 UTANGULIZI

Kumekuwa na wimbi la tuhuma za vitendo vya rushwa kwenye chaguzi mbalimbali hapa nchini na hasa baada ya kuanza kwa chaguzi za vyama vingi hapa nchini mwaka 1995. Hivyo basi ni muhimu kufahamu sheria mbalimbali ambazo zinaelezea maswala ya rushwa katika chaguzi. Sheria zinazohusika moja kwa moja na vitendo vya rushwa katika chaguzi ni zifuatazo:-

1. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya 2007 (PCCA)
2. Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa namba 1 ya 1985 (National Elections Act)
3. Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa namba 4 ya 1979 (Local Government Elections Act).

2.0. ISEMavyo SHERIA YA UCHAGUZI WA KITAIFA NAMBA 1 YA 1995 KUHUSU MAKOSA YA RUSHWA KATIKA UCHAGUZI

Sheria hii inahusika na kuongoza chaguzi za Rais, Wabunge na Madiwani. Sheria hii inatoa taratibu na mamlaka mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

2.1. USHAWISHI WA RUSHWA KUJIONDOA KUGOMBEA

Kwenye kifungu cha 112 mtu atakuwa ametenda vitendo vya rushwa endapo atamshawishi au kumnunua mtu mwingine ili ajiondoe kugombea kwenye uchaguzi. Mtu akipatikana na kosa hilo la kujiondoa na kumshawishi au kumnunua mwingine ajiondoe na akatiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka mitano (5)



2.2. ADHABU KWA HONGO, KUKIRIMU NA KUSHINIKIZA

Kifungu cha 102 kinaelezea kuwa mtu atakayetenda kosa la kutoa hongo kukirimu au kushinikiza atakuwa ametenda kitendo cha rushwa na akatiwa hatiani atapigwa faini isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano au kifungo kisichozidi miaka mitano (5) au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mtu atachukuliwa kuwa ana hatia ya hongo iwapo:

- i) Kabla au wakati wa kampeni yeye au kwa kutumia mtu mwingine alitoa, alikopesha, alikubali au kununua au kuahidi fedha yeyote au kitu cha thamani kwa mpiga kura au mtu yeyote kwa niaba ya mpiga kura ili apigiwe kura au kuzuia kupiga kura.
- ii) Kabla au wakati wa kampeni wakala wake/chama chake kwa niaba yake kikitoa au kununua au kukubali kutoa upendeleo wa kitu au masilahi ya aina yeyote kwa mpiga kura au mtu yeyote kwa niaba ya mpiga kura ili kumshawishi kupiga au kuacha kupiga kura
- iii) Kabla au wakati wa uchaguzi kwa yeye mwenyewe au kutumia wakala wake au chama chake kwa niaba yake wakatoa zawadi au ahadi, mkopo, kununua au mkataba kwa mtu yeyote kumshawishi au kununa uteuzi wa mtu kama mgombea wa chama au uchaguzi wa mtu yeyote kama mbunge.
- iv) Kwa kupata zawadi, ahadi, mkopo, mkataba, akanunua/akajihusisha kwenye ahadi au juhudzi za kununua uteuzi wa mtu kama mgombea wa chama kwa matarajio ya kupigiwa kura.
- v) Kwa madhumuni ya kuwezesha kampeni za uchaguzi au wakati wa uchaguzi kutoa fedha kwa matumizi ya mtu mwingine yeyote kwa nia ya kuhonga katika uchaguzi.
- vi) Mpiga kura yeyote kabla au wakati wa uchaguzi kwa yeye mwenyewe au kutumia mtu mwingine akapokea au akakubali kupokea fedha au kitu cha thamani kwa ajili yake au mtu mwingine yeyote ili kupiga kura au kuacha kupiga kura kwenye kura.
- vii) Baada ya uchaguzi yeye mwenyewe au mtu mwingine yeyote kwa niaba yake kupokea fedha au thamani kwa nia ya kumshukuru kwa kupiga kura au kuacha kupiga kura.

ANGALIZO: Pale ambapo kuna tuhuma kuwa hongo imetendeka na wakala au mtu yeyote kwa niaba ya mgombea itakuwa ni utetezi kwa mgombea kama atathibitisha kuwa kitendo hicho kilifanyika bila ufahamu, idhini au ridhaa yake.

KOSA LA KUKIRIMU

Kifungu cha 115 kimegusia kosa la kukirimu ambalo linafafanuliwa na kifungu cha 119. Mtu atakuwa ametenda kosa la kukirimu kwa kufanya yafuatayo:-

- a) Mtu yeyote yeye mwenyewe au mtu mwingine yeyote kabla, wakati au baada ya uchaguzi kutoa au kulipa gharama yote au sehemu ya gharama ya chakula, vinywaji na viburudisho kwa nia ya kumshawishi mtu huyo au mtu mwingine yeyote kupiga kura au kuacha kupiga kura.
- b) Mtu yeyote kukubali au kuchukua chakula, vinywaji au viburudisho.

2.3. KOSA LA VITENDO VYA RUSHWA NA UVUNJAJI SHERIA

Katika kifungu cha 117 mtu ambaye atapatikana na kosa la kitendo cha rushwa au kutenda kinyume na sheria na ambaye hukumu yake hajatenguliwa na mahakama pamoja na adhabu nyingine hataruhusiwa kupiga kura kwa kipindi cha miaka mitano toka alipohukumiwa.



Kesi ya Takrima

Sheria hii ilipelekea kesi maarufu kama Kesi ya Takrima ambayo ilifunguliwa kwa maombi yaliyowasilishwa mahakamani na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) na National Organisation for Legal Assistance (NOLA). Maombi yalifunguliwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyopelekwa mahakamani September, 2005 na kupewa namba 77 ya Mwaka 2005.

Tarehe 25 Mwezi April, 2006 Mahakama Kuu – Dar es Salaam katika maamuzi yaliyotolewa na majaji watatu ilifuta vifungu vya Sheria ya Uchaguzi wa Taifa kwa kukinzana na katiba na kuwa vya kibaguzi. Kifungu cha 119 (2) na (3) ambavyo vilikuwa vinahalalisha takrima, pamoja na kifungu 130 (b) na (c) kwa pamoja na vifungu vilifutwa na mahakama kwa kile ilichokiona kuwa kama vitaachwa vingesababisha utata kwenye kubatilisha kifungu cha 119 (2) na (3) ya Sheria hiyo.

Hukumu hiyo iliyosomwa na Jaji Nathalia Kimaro, Salum Massati na Thomas Mihayo ilisema kuwa kifungu hicho kilikuwa ni cha kibaguzi na kinakiuka Katiba ibara ya 13 (1) inayoweka misingi ya usawa mbele ya sheria na Ibara ya 21(1) inayotoa haki kwa kila raia wa Tanznia kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi.

Wakati Kifungu cha 119 (1) kinakataza vitendo vya Takrima ambavyo ni sawa na vitendo vya rushwa au uvunjaji sheria kwenye uchaguzi, kifungu hicho katika kifungu kidogo cha (2) na (3) kinahalalisha vitendo hivyo kwa namna nyingine. Hii ni kwa (1) kuhalalisha vitendo vya takrima kwa kuruhusu kukirimu watu kwa nia nzuri ambapo kifungu kidogo (3) kinasema gharama za kawaida ambazo hutumika kwa nia nzuri wakati wa kampeni za uchaguzi. Gharama hizi ni pamoja na gharama za chakula, vinywaji na burudani kutochukuliwa kama vitendo vinavyohusiana na rushwa au kwenda kinyume na sheria.

Vifungu hivyo vimefutwa pamoja na kifungu cha 130 (a) na (b) ambavyo vinaruhusu mahakama kuhalalisha vitendo vya mgombea au wakala wake kufanya vitendo vya rushwa au uvunjaji sheria kama vitakuwa vimefanyika kwa nia nzuri, ukarimu wa kawaida au gharama za kawaida za uchaguzi.

2.4. VITENDO VYA RUSHWA NA UVUNJAJI SHERIA

Kifungu cha 123 kimeainisha kuwa kila mtu

- a) Ambaye atachagua au kujaribu kuchagua au kushawishi au kununua watu wengine kupiga kura katika uchaguzi wowote ikiwa yeye kwa ufahamu wake huyo mtu mwingine ameshapiga kura katika uchaguzi atakuwa amefanya kitendo cha rushwa.
- b) Ambaye kwa madhumuni ya kununua karatasi ya kupigia kura kwa mtu mwingine au yeye mwenyewe au kutoa shahada yeyote iliyotolewa kwake au kwa watu wengine au kushawishi au kununua watu wengine kutoa shahada za watu hao wengine kwa yeye au kwa watu wengine atakuwa amefanya kosa la kitendo cha rushwa.



Kwa makosa yaliyoainishwa hapo juu kwenye a) na b) mtu huyo akikutwa na hatia atapigwa faini ya shilingi za kitanzania laki Tano au kifungo kisichozidi miaka mitano (5) au adhabu zote mbili kwa pamoja.

2.5. HONGO, KUKIRIMU AU KUSHAWISHI KUNAKOHUSISHA WAJUMBE AU MAAFISA WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

Kifungu cha 121 kinaeleza pale ambapo mtu yeyote anafanya kitendo kilichoainishwa kwenye kifungu cha 118, 119 na 120 (vilivyojadiliwa hapo juu) kwa mjumbe au afisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa nia ya mtu huyo kubagua ili kumfaidisha mgombea mmoja au wengine katika uchaguzi au ambapo mjumbe yeyote au afisa vitendo hivyo kwa nia ya kabagua kumfaidisha mgombea mmoja au mwingine mtu huyo atakuwa na kosa la hongo, kukirimu au kushinikiza.

2.6. KUONDOLEWA KWENYE DAFTARI KWA WALIOTIWA HATIANI

Pale ambapo mahakama imemtia hatiani mtu kwa vitendo vya rushwa na kuvunja sheria kifungu cha 128 kinataka taarifa ya kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ili kama mtu huyo aliyetiwa hatiani ameandikishwa kama mpiga kura aondolewe kwenye daftari la wapiga kura

2.7. MAKOSA KWA MAAFISA WA UCHAGUZI

Katika kifungu cha 131 Pale ambapo kwenye uchaguzi imethibitishwa makosa ya rushwa, kukirimu na vitendo vya uvunjaji sheria vilijulikana kutendeka na vikawezeshwa na mjumbe au Afisa wa Tume au mtu mwingine anayefanya kwa maelekezo ya tume, mjumbe au Afisa au mtu mwingine atakuwa na kosa na atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka mitano (5).

2.8. TAARIFA YA MAHAKAMA KUU KWA MKURUGENZI WA UCHAGUZI KUHUSU VITENDO VYA RUSHWA NA UVUNJAJI SHERIA

Kifungu cha 136 pale ambapo Mahakama imemkuta mtuhumiwa na hatia za rushwa na vitendo vya uvunjaji sheria itamtaarifu Mkurugenzi wa Uchaguzi na kama mtu huyo ameandikishwa kupiga kura atamfuta jina lake kwenye daftari la wapiga kura.

Baada ya kumalizika kesi ya uchaguzi mahakama itathibitisha kwa Mkurugenzi wa uchaguzi yafuatayo:-

- i) Kama kuna kosa la rushwa au uvunjaji wa sheria limethibitishwa kufanywa na mgombea au kwa ufahamu, idhini au ridhaa ya mgombea huyo.
- ii) Baada ya mtuhumiwa kutiwa hatiani na mahakama kuthibitisha kwamba rushwa au uvunjaji wa sheria umetendeka kwa ufahamu, ridhaa na idhini ya mgombea pamoja na adhabu nyingine, mgombea atapoteza sifa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atachapisha shahada ya mahakama kwenye gazeti la serikali na kufuta jina la Mgombea kwenye daftari la wapiga kura.

3.0. ISEMAVYO SHERIA YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA NAMBA 4 YA 1979 KUHUSU RUSHWA KATIKA UCHAGUZI

Sheria inaongoza uchaguzi wa serikali za mitaa ambao unawachagua wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji pamoja wajumbe wa mitaa na vijiji.

3.1. ADHABU KWA WATU WANAOVUNJA SHERIA

Kifungu cha 106 kinaainisha kuwa kila mtu:-

- a) Anayepiga au anayejaribu kupiga kura au kushawishi au kununua watu wengine kupiga kura kwenye uchaguzi wowote huku akiwa anajua watu hao wengine wameshapiga kura kwenye uchaguzi huo au mwingine.
- b) Kwa madhumuni ya kununua karatasi ya kupiga kura kwa mtu mwingine au kwa ajili yake au akashawishi au kununua watu wengine kukabidhi shahada zao kwa watu wengine.

3.2. WATUHUMIWA WALIOPATIKANA NA HATIA ZA RUSHWA NA UVUNJAJI SHERIA KUONDOLEWA KWENYE DAFTARI

Kifungu cha 111 kinaainisha kuwa pale ambapo mahakama inamtia hatiani kwa vitendo vya rushwa au uvunjaji wa sheria inatoa taarifa ya hatia hiyo kwa afisa mwandikishaji wa kata yeoyote ambapo ana sababu ya kuamini mtu huyo ameandikishwa. Pale ambapo afisa mwandikishaji anapokea taarifa hiyo kwa mujibu wa kifungu hiki anatakiwa mara moja kuondoa jina kwenye daftari la wapiga kura.

4.0. ISEMAVYO SHERIA NAMBA 11 YA 2007 KUHUSU MAKOSA YA RUSHWA KATIKA CHAGUZI



4.1. HONGO NA VITENDO VYA RUSHWA

Kifungu cha 15 cha sheria hii vitendo / makosa ya hongo na rushwa yanaweza kufanywa na mtu mwenyewe au kwa kushirikiana na mtu mwingine kwa namna zifuatazo:-

Kushawishi, kupokea au kupata au kujaribu kupata, kutoa ahadi, au kuahidi manufaa kutoka kwa mtu yejote kwa ajili yake mwenyewe au kwa ajili ya mtu mwingine manufaa, ushawishi, zawadi au vinginevyo kwa jambo linalohusiana na mwajiri wake.

Mtu akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania kati ya laki tano na milioni moja au kifungo cha kati ya miaka mitatu hadi mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.2. RUSHWA YA NGONO

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha sheria hii ni kosa kwa mtu mwenye mamlaka kudai au kuomba rushwa ya ngono kwa mtu yeyote kama sharti la kutoa ajira, upendeleo, kumpandisha cheo, kumpatia haki au huduma maalumu.

Mtu akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania isiyozidi milioni tano au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.3. KUSHIRIKI NA KUSAIDIA KUTENDA UOVU

Mtu yeyote ambaye anamsaidia na kwa makusudi mtu mwingine kutenda maovu chini ya kifungu cha 30 cha sheria hii anakuwa anatenda kosa.

Mtu akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania isiyozidi milioni mbili au kifungo cha miaka isiyozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.4. MATUMIZI MABAYA YA MAMLAKA

Kutumia vibaya na kwa makusudi nafasi au madaraka uliyonayo katika kutenda au kutotenda na kuvunja sheria katika utendaji wako wa kazi kwa kutumia cheo au nafasi yako ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha sheria hii.

Mtu akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania isiyozidi milioni tano au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.5. KULA NJAMA

Ni kosa chini ya kifungu cha 32 cha sheria hii kwa mtu yeyote kula njama na mtu mwingine kutenda kosa.

Mtu akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania isiyozidi milioni tano au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.6. KUTUMIA USHAWISHI

Mtu yeote ambaye anaahidi au kutoa au kumpatia Afisa yeote wa umma, au Afisa wa umma kudai au kupokea manufaa yeote yasiyo halali ili atumie vibaya nafasi yake au ushawishi wake kwa lengo la kumpatia manufaa yasiyo halali mtu huyo kutoka kwa utawala au mamlaka ya umma atakuwa ametenda kosa chini ya kifungu cha 33 cha sheria hii.

Mtu yoyote akipatikana na hatia kwa makosa haya atastahili adhabu ya faini fedha za kitanzania isiyozidi milioni tatu au kifungo cha miaka isiyozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.



5.0. ANUANI ZA OFISI ZA TAKUKURU ZA MIKOZA NA WILAYA

Tumeweka anuani hizi na simu ili kukuwezesha wewe mwananchi mtanzania wa kawaida ukiwa na tatizo ambalo linahitaji kushughulikiwa na TAKUKURU piga simu kwenye ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe au piga Hotline ya TAKUKURU 113.

MAKAO MAKUU TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA ANUANI ZA OFISI ZA TAKUKURU ZA MIKOZA NA WILAYA

REGION/DISTRCT	BOX	TELEPHONE	MOBILE	FAX	EMAIL
PCCB HEAD QUARTER	4865	022 2150043-6		022 2150047	dgeneral@pccb.go.tz
ARUSHA	1055	027 2503538/027 2507928	0784 329431	027 2505973	pcb-ar@habari.co.tz
KARATU	208	027 2534443		(027)2534443	
NGORONGORO	1055	027 2535224		(027)2535224	
MONDULI	85	027 2538340		(027)2535340	
ARUMERU	724	027 2553729		(027)2553711	
LONGIDO	3		0784407661, 0713 407661		
DAR ES SALAAM	6420	022 2132954	0786 733567	022 2123019	
ILALA	6420	022 2861088	0754 098 530		
KINONDONI	90397	022 2170852	0754 325858		
TEMEKE	42325	022 2863092	0784 761473		
DODOMA	1175	026 2322846, 026 2322003	0784 998802	026 2320003	
MPWAPWA	212	026 2320712			
BAHI	1175	026 2321979			
CHAMWINO	1175	026 2321979.			
KONDOA	710	026 2360203			
KONGWA	176	026 2320586			
IRINGA	1575	026 2701700, 026 2700156	0784 998811	026 2703014	Pcb@iringanet.com
KILOLO	2300		0754640235		
LUDEWA	146	026 2790046			
MUFINDI	303	026 2772476			
MAKETE	104	026 2740167			
NJOMBE	629	026 27877			
KAGERA	1138	028 2220848	0784 998826		
BIHARAMULO	179	028 2223518			
KARAGWE	41	028 2222248			
MULEBA	19	028 2222700			
NGARA	6	0288 2223664		0282223664	
KIGOMA	880	028 2802899	0784 654849	028 2804928	
KASULU	111	028 - 2810609			
KIBONDO	125	028 2820412			
KILIMANJARO	1951	027 2750885/9	0784 407946	027 2750885	pcbkili@kilionline.com
HAI	309	0272757025		0272757025	
MWANGA	310	022756268		022756268	
ROMBO	321	027 2758985		027 2758985	
SAME	154	027 2758 422		027 2758 422	
SIHA	156	027 2758911		027 2758911	
LINDI	1004	023 2202456, 023 2202799.	0786: 733563	023 22022215	
KILWA	91	023 2013053		023 2013053	
LIWALE	101		0741771047		
NACHINGWEA		023 2933125	0784860996	023 2933125	
RUANGWA	53	023 293261	07548004442	023 293261	
MARA	377	028 2620240	0786 733569	028 2620012	pcbmusoma@juasun.net This e-mail address is being protected from spambots. You need JavaScript enabled to view it
BUNDA	178	028 2621320		028 261320	
MUSOMA VIJJINI	263	028 2622744			
SERENGETI	149	028 2621625		028 2621625	
TARIME	277	028 2690697		028 2690697	

MANYARA	386	027 2530255/6	0786 733562	027 2530448	pcbmanyara@africaonline.co.tz This e-mail address is being protected from spambots. You need JavaScript enabled to view it
HANAN'G	158	027 2531679		027 2531679	
KITETO	120	0272555382		0272555382	
MBULU	239	027 2533027		027 2533027	
SIMANJIRO	9500	027 2555639		027 2555639	
MBEYA	1419	025 2503566	0784 998846	025 25029	
CHUNYA	72	025 2520231		025 2520231	
ILEJE	36	025 2570132		025 2570132	
KYELA	578	025 2540083			
MBARALI	228	025 2590082		025 2590083	
MBOZI	588	025 2580226		025 2580226	
RUNGWE	328	025 2552109		025 2552109	
MOROGORO	845	023 2614203, 023 2614478	0784 998845	023 2604478	Pcb-moro@morogoro.net
IFAKARA/ KILOMBERO	579	023 2625386		023 2625386	
KILOSA	154	023 2623449		023 2623086	
MVOMERO	6091	023 2600537		023 2600537	
ULANGA	130	023 2604478	0784 998845	023 2627031	
MTWARA	213	023- 2334013, 023 2333726	0784 998847	023 2334013	pcbmtr@makondenet.com
MASASI	214	023- 2510553		023- 2510553	
NANYUMBU	214		0786 733337		
NEWALA	176	023- 2410626		023- 2410626	
TANDAHIMBA	12	023- 2410033.		023- 2410033	
RUKWA	273	025 2802426, 025 2802926	0784 222664	025 2800312	
MPANDA	275	025 2820613			
NKASI	01	025 280293		025 2830124	
RUVUMA		025 2600613	0784 998839	025 2600663	pcbruv@africaonline.co.tz This e-mail address is being protected from spambots. You need JavaScript enabled to view it
MBINGA	285	025 2640686		025 2640686	
NAMTUMBO	5	025 2602898		025 2602892	
TUNDURU	147	025 2680342		025 2680340	
SHINYANGA	37	028 2762630	0784 998803	028 2763358	pcbshy@yahoo.co.uk
BARIADI	306	028 2700371		028 2700532	
BUKOMBE	139	028 2555508		028 7342520	
KAHAMA	538	028 2710936		028 2763358	
KISHAPU	9		0787 973912		
MASWA	315	028 2750008,133		028 275000	
MEATU	119	028 2795120,133		028 2795120	
SINGIDA	484	026 2502305	0787 861516	026 2502550	pcbsingida@africaonline.co.tz
IRAMBA	139	026 2502370		026 2502550	
MANYONI	13	026 2540277		026 2540275	
TABORA	1020	026 04311/2604030	0784 329434	026 2604039	pcbtbr@taboraonline.co.tz
IGUNGA	220	026 50294		026 2650294	
NZEGA	56	026 92331		026 92331	
SIKONGE	106	026 04287		026 988242	
URAMBO	132	0262604287		0732 988254	
UYUI	18800	026 2605311		026 2605311	
TANGA	1953	027 2645186	0787 762435	027 2647885	
HANDENI	386	027 2641772	0784 430440		
KILINDI	55		0784 455805, 0713448460.		
KOROGWE	412	027 2640598	0784 384245, 071384245		
LUSHOTO	302	027 2640268	0784 428183		
MKINGA			0784 478637, 0713474459		
MUHEZA	270	027 2641221	0784 478707, 0713478707		
COASTAL REGION	30261	023 240265	0786 733563	023 2402657	pcbpwani@africaonline.co.tz
BAGAMOYO	262	023 2440105			
KISARAWE	28082	023 2402760			023 2402766
MAFIA	76	023 2010179		023 2010179	023 2010179
MKURANGA	102	0754 801261			023 2010750
RUFIFI	18	023 2010293			023 2010365

Serikali ya Tanzania katika mkakati wa pili wa kupambana na rushwa yaani NACSAP II (2006-2011) imesitisiza juu ya umuhimu wa ushiriki wa wadau wote katika mapambano dhidi ya rushwa hasa mashirika yasiyo ya kiserikali, Sekta binafsi, vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla.

Hivyo jukumu la kupambana na rushwa hapa Tanzania ni la kila mtu na ili uweze kupambana na rushwa lazima uwe nauelewa wa mambo mbalimbali zikiwemo sheria mbalimbali zinazohusu rushwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo sheria namba 11 ya 2007.

Kitabu hiki cha pili ni muendelezo wa juhudi za pamoja kati ya Policy Forum na TAKUKURU kutoa elimu kwa umma juu ya sheria zisemavyo kuhusu makosa ya rushwa katika chaguzi zetu na adhabu zinazotolewa kwa makosa hayo.

Mkakati wa serikali wa kupambana na rushwa awamu ya pili (NACSAP II) umejielekeza zaidi na kuweka nguvu sana katika kukinga kwa maana ya kuelimisha umma ili watu wasifanye makosa ya rushwa pasipo kujua. Kusudi la mkakati huu pia ni kuondoa lawama ili asiwepo mtu atakayesema kuwa hakujuua ndio maana alifanya makosa husika.



Urambo - Kalenga RD. Upanga
S.L.P4865. Dar es Salaam. Tanzania
Tel: +255 22 2150043-6. Fax: +255 22 2150047
Email: hic@pccb.go.tz
dgeneral@pccb.go.tz



policy forum

Plot 270• Kiko Avenue Mikocheni 'B'
S.L.P 38486 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu: +255 22 2772611 • Fax: +255 22 2701433,
Mob: +255 782 317 434
Barua Pepe: info@policyforum.or.tz